

MAJUKUMU SEHEMU YA USHIRIKA

- Uhamasishaji wa wananchi ili wajiunge na vyama vya Ushirika
- Kutoa elimu kwa wanachama, viongozi na watendaji wa vyama vya Ushirika
- Kukagua na kusimamia vyama vya Ushirika
- Kukusanya na kuhifadhi takwimu za vyama vya Ushirika
- Kusimamia na kuendeleza mradi wa VICOBA

FURSA SEHEMU YA USHIRIKA

- Shughuli za uvuvi, uendeshaji bodaboda, kilimo, ufugaji viwanda,taasisi, biashara mbalimbali zinafanyika ambazo ni maeneo muhimu ya kuanzishwa vyama vya ushirika.
- Maeneo ya uwekezaji kwa wanaushirika yapo kama vile Jengo la TFC Mnazi mmoja, Benki ya Ushirika Tanzania n.k
- Utaalaam upo

KITENGO CHA USHIRIKA:

1. Kukagua vyama vya ushirika vya aina zote
2. Kusimamia utekelezaji wa sera na sheria ya vyama vya ushirika
3. Kuhamasisha uanzishwaji na uendelezaji wa vyama vya ushirika
4. Kutoa ushauri katika uendeshaji wa vyama vya ushirika
5. Kuhimiza uanzishaji wa taasisi za fedha za ushirika, mfano; benki, bima, SACCOS
6. Kuhudhuria mikutano mikuu ya vyama vya Ushirika na kutoa ufafanuzi wa kisheria na uendeshaji.
7. Kusaidia kutoa maelekezo na taratibu za kuandikisha vyama vya ushirika
8. Kutatua migogoro ndani ya vyama vya ushirika
9. Kusaidia kuandaa 'by – laws' za vyama vya ushirika
10. Kusimamia na kutoa elimu ya ushirika kwa wanachama, bodi za vyama na watendaji wa vyama vya Ushirika.

11. Kutoa tathmini ya vyama vya ushirika kwa kuzingatia "viability criteria"
12. Kusimamia uchaguzi wa viongozi wa vyama vya ushirika
13. Kuhimiza na kuvishawishi vikundi vya akina mama na vijana kuanzisha vyama vya ushirika.
14. Kusaidia katika kutoa takwimu kwa ajili ya utafiti endelevu
15. Kushirikiana na taasisi mbalimbali katika kuvielekeza vyama vya ushirika kupata fedha za ununuzi wa mazao na biashara nyinginezo
16. Kutoa taarifa ya hali ya ushirika kwa viongozi wa juu kwa ajili ya hatua zingine.
17. Kuweka kumbukumbu sahihi za vyama vya ushirika katika eneo lake
18. Kushiriki katika vikao vya kitaalamu katika eneo lake
19. Kuhudhuria mahakamani kutoa ushahidi kwa kesi za wizi na ubadhilifu katika vyama vya ushirika
20. Kuviunganisha vyama vya Ushirika na wabia au wafanya biashara wengine katika kuingia mikataba kwa manufaa ya vyama vya Ushirika.
21. Kusimamia ajira za watumishi wa vyama vya ushirika
22. Kusaidia kutoa tafsiri sahihi ya hesabu zilizokaguliwa kwa wanachama na Halmashauri za vyama vya ushirika
23. Kuwa wasimamizi wa ufilisi wa vyama ambavyo vinashindwa kufanya kazi na kulazimisha kufilisiwa.
24. Kutoa taarifa zozote muhimu kwa ajili ya maendeleo ya ushirika
25. Kutekeleza na kuzingatia Nyaraka za Mrajis zitakazo gusa eneo lake la kazi.